# OFIS YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
# HALMASHAURI YA WILAYA YA MPIMBWE
# SHULE YA SEKONDARI MAMBA

BARUA PEPE: mambaseco@gmail.com .
SIMU: 0754441413/0622031594 .

SHULE YA SEKONDARI MAMBA,
S.L.P 93,
MPANDA – KATAVI,
……../……../…………

Ndg. Mzazi/mlezi wa,

……………………………………………………………………………………….

**YAH: MAELEKEZO YA MWANAO KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA (I) KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAMBA.**

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu.

Ninayofuraha kubwa kukufahamisha kuwa mwanao aliyetajwa hapo juu ni miongoni mwa vijana wachache waliopata bahati/fursa ya kuendelea na masomo ya kidato cha kwanza mwaka ……… katika shule ya **SEKONDARI MAMBA**.

Kwa barua hii nakuarifu kuwa nakala ya fomu ya kujiunga na shule ya sekondari Mamba, mwanao ataipata shuleni alikomalizia darasa la saba na utalazamika kuizalisha ili uweze kupata nakala yako ambayo itakuongoza kumtimizia mwanao mahitaji muhimu, kisha utajaza sehemu zinazotakiwa kujaza na kuirejesha hapa shuleni siku ya kuripoti.

Pamoja na kuyasoma kwa kina naomba uendelee kumshauri mwanao juu ya kutumia vema nafasi hii aliyoipata ili lengo na azma yake itimie. Tarehe ya kumleta mwanao hapa shuleni ni ……………….. na mwisho wa kuripoti itakuwa tarehe…………………….. Tafadhari fika kwa wakati siku na muda wa kazi ili kuepuka usumbufu.

Nakutakia maandalizi mema na karibu sana mamba sekondari.

Wako,

……………………….

**SAMWEL S. LYOBA**

MKUU WA SHULE

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAMBA**

Mambo muhimu ya kuzingatia:

(A) SARE ZA SHULE

❖ **WAVULANA**

- Suruali mbili (02) za rangi ya dark bluu inatakiwa iwe inchi 21 kwenye mkunjo wa chini (turn up), isiyobana makalio, mifuko miwili mbele (sio kama jinsi) na mfuko mmoja nyuma.
- Suruali moja ya kijani rangi ya mgomba.
- Mashati mawili meupe-mikono mifupi.
- Fulana (T-shirt) ya bluu bahari. Hii inapatikana shuleni.
- Vitu vya ngozi nyeusi vyenye Kamba na visigino vifupi (***sio raba wala yeboyebo***)
- Sweta rangi ya bluu "V" (Makoti hayaruhusiwi)
- Soksi nyeusi ndefu jozi mbili.

❖ **WASICHANA**

- Sketi mbili (02) za rangi ya dark bluu, zinatakiwa ziwe na urefu unafika kwenye kifundo cha mguu, mshono wa sketi ni RINDA BOX iwe na mfuko mmoja kulia na zipu na huksi upande wa kushoto.
- Gauni moja ya kijani rangi ya mgomba, yenye urefu unaofika kwenye kifundo cha mguu. (***Mwanafunzi haruhusiwi kushona shamba dress ya sketi akifanya hivyo hatopokelewa***)
- Mashati mawili meupe-mikono mifupi.
- Fulana (T-shirt) ya bluu bahari. Hii inapatikana shuleni.
- Vitu vya ngozi nyeusi vyenye Kamba na visigino vifupi (***sio raba wala yeboyebo***)
- Sweta rangi ya bluu "V" (Makoti hayaruhusiwi)
- Soksi nyeupe ndefu jozi mbili.

(B) MAVAZI YA MICHEZO.

- Viatu (raba) vya michezo vya aina au rangi yoyote.
- Fulana nyeusi yenye kola na mistari myeupe pembeni (Track)
- Suluari nyeusi ya track yenye mistari myeupe pembeni.

NB:

"N***guo zingine tofauti na zilizoainishwa hapo juu katika fomu hii haziruhusiwi, hivyo mwanafunzi hatakiwi kuja nazo***"

**(C) VIFAA VINGINE**.

- Daftari kumi na moja (Kaunta book 3 quire), kalamu na mkebe wa hisabati
- Vifaa vya usafi : Ndoo ya lita kumi, Fagio la chelewa, Jembe jipya lenye mpini (kwa wavulana), Fyekeo au panga (kwa wasichana)

## (D) MAHITAJI KWA WANAFUNZI WA HOSTELI

Shule ina nafasi chache za hosteli kwa wavulana na wasichana, hivyo watakaopata nafasi hii ni walae watakaofika mapema na kulipia michango yao yote kwa wakati.

(i) Mahindi debe tatu (03) kwa miezi sita (muhula) au gunia moja (Debe 06) kwa mwaka.
(ii) Maharage debe $1\frac{1}{2}$ kwa miezi sita (muhula) au debe 03 kwa mwaka (mihula miwili)
(iii) Mchele debe moja kwa miezi sita (muhula) au Debe mbili (02) kwa mwaka (mihula miwili)
(iv) Pesa shilingi za kitanzania elfu hamsini (50,000/=) kwa miezi sita au laki moja (100,000/=) kwa mwaka (mihula miwili).
(v) Shuka mbili za bluu bahari, mto na foronya lake na taulo/kitenge (kwa wasichana) kwa ajili ya kuogea.
(vi) Sanduku imara la kuwekea vitu vyake (Tranka).
(vii) Godoro la ukubwa wa futi $2\frac{1}{2}$ kwa futi 06.
(viii) Sahani, Bakuli, Kikombe, na Kijiko kwa ajili ya chakula.
(ix) Ndala za kuogea.
(x) Chandarua cha pande nne na sio cha duara/ mviringo kwa juu.
(xi) Ndoo mbili zenye ujazo wa lita kumi.

## CHAKULA CHA MCHANA KWA WANAFUNZI WA KUTWA.

Serikali imeagiza kuwa wanafunzi wote wa kutwa (wanaokuja shuleni na kurudi nyumbani baada ya masomo) wale chakula cha mchana shuleni. Hivyo kila mwanafunzi wa kutwa atatakiwa alete mahitaji yafuatayo.

(a) Mahindi debe mbili (kg 40)
(b) Maharage sado 03.
(c) Fedha shilingi za kitanzania elfu thelathini (30,000/=)

## 1.0 **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia Na. 5 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sharia Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu, sayansi, na Teknolojia, yenye dhamana ya elimu chini ya ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi wa uendeshaji Elimu.

2.1 Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuwasili shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani nan je ya shule kulinganba na ratiba ya shule ni jambo la lazima;

(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio binafsi ya jioni (Night preparation) ni lazima;
(d) Kuwahi katika shughuli nyingine za shule utakazopewa
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule ni jambo la lazima.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa na hasa uwapo shuleni na unaposafiri (Wanafunzi wa Hosteli)
(h) Kuzingatia ratiba ya shule
(i) Kutunza mali za umma.

**2.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:**

(i) Wizi
(ii) Uasherati na ushoga
(iii) Ubakaji
(iv) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji sigara, Bangi, Cocaine, mirungi, Kubeli na kadhalika.
(v) Kupigana au kupiga.
(vi) Kuharibu kwa maksudi mali ya umma.
(vii) Kudharau bendera ya Taifa.
(viii) Kuwa mjamzito/kupata mimba/kusababisha mimba.
(ix) Kuoa au kuolewa.
(x) Kutoa mimba
(xi) Kugoma, kuchochea au kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu.
(xii) Kukataa adhabu kwa maksudi.
(xiii) Kumiliki, kutumia au kukutwa na SIMU (***Endapo mwanafunzi atakutwa na SIMU, simu hiyo itachukuliwa na Hatorudishiwa kamwe bila kujali ni ya nani***)

**Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi**

(a) Medical examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali au Kituo cha Afya. **Zahanati haziruhusiwi**.
(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makossa ya jinai.
(c) Kivuli cha cheti cha kuzaliwa.

## SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**TO THE MEDICAL OFFICER**

**……………………………………………………………..**

Name of student……………………………………………..

Form…………………………..term…………………..year……………………….

Dear doctor,

Please kindly examine the above named student to prove his/her fitness undertaking studies at our school.

1. X – Ray ( ) 2 Urine ( ) 3. Stool ( )
4. Physical fitness ( ) 5. V. D ( ) 6. Tuberculosis ( )

A (i) **PRELIMINARY INFORMATION (BY THE STUDENT BEFORE THE DOCTOR**)

| NO. | DISEASE | YES/NO | NO. | DESEASE | YES/NO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuberculosis | | 10 | Epilepsy | |
| 2 | Pneumonia | | 11 | Ear, Nose and Threat | |
| 3 | Asthma | | 12 | Skin Disorder Disease | |
| 4 | Heart trouble | | 13 | Armenia | |
| 5 | Recurrent indigestion | | 14 | Operation | |
| 6 | Jaundice | | 15 | Malaria | |
| 7 | dysentery | | 16 | Stomach trouble | |
| 8 | Kidney and urinary trouble | | 17 | Serious Accident | |
| 9 | Nervous breakdown | | 18 | Eye disorder | |

(ii) **VACCINATION AND INNOVOLULATIONS HISTORY**

| **DISEASE** | **1st DATE** | **2nd DATE** | **3rd DATE** |
|---|---|---|---|
| Small pox | | | |
| Whooping Cough | | | |
| Measles | | | |
| Yellow Fever | | | |
| Cholera | | | |

(a) Weight………………….

(b) heart beat…………………..

(c) Vision……………………..

## MEDICAL CERTIFICATION

I have examined the above and considered that he/she is physically fit/unfit to undergo studies.

(****Delete whichever unnecessary***)

DOCTOR'S NAME & SIGNATURE…………………………………………………

DATE…………………………………………….

**UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI**

Mimi………………………………………………………………..nikiwa na akili timamu nakiri kuwa nimesoma sharia, kanuni na taratibu za shule kwa umakini na utulivu mkubwa. Hivyo basi naahidi:

"***Nitazifuata sharia, Kanuni na taratibu zote za shule kama zilivyoelekeza. Aidha ninaamini kuwa sharia na Taratibu zote zipo kwa nia ya kunisaidia katika Nyanja zote muhimu ikiwa ni pamoja na nidhamu na taalum****a*". Kinyume na hivyo Hatua sitahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu.

Jina la mwanafunzi…………………………………………………………….

Tarehe………………………………………….Saini……………………….

Jina la mzazi/Mlezi…………………………………………………………………

Tarehe ………………………………..Saini………………………………

****Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakapowasili shuleni***.

**KARIBU SANA MAMBA SEKONDARI**

**……………………………..**

SAMWEL S. LYOBA
MKUU WA SHULE